

Nauli za Abiria na Mizigo katika Njia ya Kiwira-Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa

TANGAZO LA SERIKALI NA 623 la tarehe 01/09/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA NA MIZIGO KATIKA NJIA YA KIWIRA-MBAMBA BAY
KATIKA ZIWA NYASA YA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

- Jina **1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria na Mizigo Katika Njia ya Kiwira-Mbamba Bay Katika Ziwa Nyasa ya Mwaka 2023.
- Matumizi **2.** Amri hii itatumiwa na meli zinazomilikiwa na Kampuni wakati zikitoa huduma ya usafirishaji abiria na mizigo maeneo ya Tanzania katika Ziwa Nyasa.
- Tafsiri **3.** Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
- Sura ya 415 “Sheria” maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;
- Sura ya 212 “Kampuni” maana yake ni Kampuni ya Huduma za Meli iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni;
- “Shirika” maana yake Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;
- “meli” maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika Ziwa Nyasa.

SEHEMU YA PILI
NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

Nauli
zilizoidhini
shwa

4. Kampuni inayoendesha meli-

- (a) itatoza nauli ya abiria na mizigo isiyozidi viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili katika Amri hii;
- (b) itatunza taarifa za ubebaji wa abiria na mizigo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo udhibiti;
- (c) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyotolewa na Shirika kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini.

Sura ya
165

Masharti
ya huduma

5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:

- (a) itatoa tiketi kwa abiria zinazoonesha nauli isiyozidi viwango vilivyoainishwa;
- (b) itatoa tiketi kwa abiria wakiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;
- (c) itapima uzito wa mizigo ikiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;
- (d) itazingatia ratiba ya safari za meli kama ilivyotolewa na kampuni kwa wateja; na
- (e) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake.

Sura ya
165

Nauli za Abiria na Mizigo katika Njia ya Kiwira-Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa

TANGAZO LA SERIKALI NA. 623 (Linaendelea)

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya 4(a))

NAULI KIKOMO ZA ABIRIA ZILIZOIDHINISHWA KWA AJILI YA NJIA YA KIWIRA-MBAMBA BAY

Njia	VIP I (TZS)	VIP II (TZS)	DARAJA LA PILI (TZS)	DARAJA LA FATU (TZS)
Kiwira – Ifungu	18,600	16,600	10,800	4,500
Kiwira – Manda	27,900	20,600	15,600	9,600
Kiwira – Mkili	33,200	26,600	18,600	10,900
Kiwira - Mbamba Bay	45,600	35,800	25,600	17,300
Nsisi – Manda	18,600	16,600	10,800	5,800
Nsisi – Mkili	27,900	24,800	18,600	8,300
Nsisi - Mbamba Bay	35,800	30,600	21,900	10,900
Manda – Mkili	18,600	16,600	10,800	5,800
Manda - Mbamba Bay	27,900	20,600	18,600	9,600
Njambe - Mbamba Bay	18,600	16,600	10,800	4,500

Nauli za Abiria na Mizigo katika Njia ya Kiwira-Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa

TANGAZO LA SERIKALI NA. 623 (Linaendelea)

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya 4(a))

**NAULI KIKOMO ZA MIZIGO ZILIZOIDHINISHWA KWA AJILI YA NJIA YA
KIWIRA-MBAMBA BAY**

Bidhaa	Kipimo	Kiwango (Tsh)
Kichele/ Bidhaa zinazochukua nafasi kubwa	tani	50,000
Godoro	moja	1,500
Pikipiki/Baiskeli	moja	10,000
Gari	tani	35,000
Wanyama/Ndege	kasha la wanyama	20,000
Bidhaa nyingine	tani	20,000

Dar es Salaam,
1 Agosti, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE
Mkurugenzi Mkuu